# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAISI
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**SHULE YA SEKONDARI MTWANGO**
**S.L.P 370**
**NJOMBE**

---

**Mawasiliano;**
**MKUU WA SHULE**
**Simu : 0763518938**
**NJOMBE**

**MAKAMU MKUU WA SHULE**
**Simu: 0756748912/0622730576**

**MWALIMU WA TAALUMA**
**Simu: 0769444340/0718728412**

**MWALIMU MLEZI**
**Simu: 0711516535/0762071459**

**(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe kwa Mkuu wa shule na sio mtu binafsi)**
**Unapojibu tafadhali taja;**

**Kumb.Na.MTSS/REG.NO.S.0431**
**Ndugu ……………………………………………………………………………**
**Mzazi/Mlezi …………………………………………………………………..**
**S.L.P …………………………………………………..**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya **CBG,HKL,HGL,HGK**. Shule ya sekondari MTWANGO ipo umbali wa **kilomita 25** kutoka Makambako hadi Mtwango stendi nauli yake ni **1500/=** lakini ukitokea njombe stendi hadi Mtwango stendi umbali ni **kilomita 34** nauli yake ni **1500/=** usafiri wa pikipiki nauli Tsh. 2,000/= ukitokea kituo cha mabasi Mtwango hadi shule ilipo.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ………………………………………….. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………………………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………………………..

**KAULI MBIU YA SHULE (SCHOOL MOTTO)**
**"ELIMU HAINA MWISHO"**

Kauli hiyo ndiyo dira yako utakapokuwa hapa kwa kipindi chote cha miaka miwili. Unatakiwa kuitafakari kauli hiyo kwa vitendo. Ni matumaini yetu kuwa utatumia nafasi hii adimu kwa manufaa yako na kwa Taifa kwa ujumla. Hivyo basi utatakiwa kuwa na tabia njema na uhudhurie masomo na ujifunze kwa bidii.

……………………………………………
VERONICA MFUGALE
MKUU WA SHULE

**ADA NA MICHANGO MINGINE YA SHULE**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= mwanafunzi atalipa shilingi elfu 35,000/= kwa muhula.Shule hii ni mpya hivyo akaunti ya malipoinaendelea kushugulikiwa punde ikiwa tayari Wanafunzi watajulishwa. Tafadhali andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake kwenye pay slip. Pindi afikapo shuleni awasilishe kwa mhasibu wa shule.

b) Michango mingine inayotakiwa kulipwa na kila mzazi kwa muhula wa kwanza ni:

i. Tsh. 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani (kwa mwaka)
ii. Tsh. 6,000/= kwa ajili kitambulisho
iii. Tsh. 20,000/= kwa ajili ya taaluma (kwa mwaka)
iv. Tsh. 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine (kwa mwaka)
v. Tsh. 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza (kwa mwaka)
vi. Tsh. 10,000/= tahadhali (haitarejeshwa) (kwa mwaka)
vii. Mchango wa mahafali Tsh. 10,000/= (tsh. 5,000/= kwa kila mwaka)

**(Jumla ya Ada na michango mingine ni Tsh. 171,000/=)**

**NB: Fedha zote zitalipwa kupita akaunti ya shule itakayofunguliwa.**

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni;

i. Ream za karatasi A4 2 (kila muhula atatoa Ream 1)
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biology
iv. Scientific calculator
v. Godoro la futi $2\frac{1}{2}$
vi. Mashuka pair 2 rangi ya pinki kwa wasichana na blue bahari kwa Wavulana, blanketi 1, chandarua 1, foronya na mto.
vii. Vyombo vya chakula (sahani za bati zenye patition , kijiko na kikombe)
viii. Soft broom 1 na jembe lenye mpini kwa ajili ya usafi.
ix. Ndoo mbili (1 kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi na 1 kwa ajili ya matumizi mengine)
x. Kwanja 1.
xi. Tochi ya solar kwa matumizi yake nyakati za usiku ni muhimu sana. (ingawa umeme upo).

## SARE ZA SHULE

WAVULANA

- Suruali mbili,rangi ya nyeusi upana nch 18 mifuko mitatu mbele miwili na nyuma mmoja.
- Mashati mawili meupe (mikono mirefu)
- Tai rangi nyeusi
- T – shirt (02) za ranga ya kijivu (shamba dress)
- Sweta mbili (02) rangi ya “kijani jeshi”
- Track suit 2 za rangi ya kijivu.(isiwe ya kofia) kwani hali ya hewa ya mtwango ni baridi kali
- Suruali mbili,rangi ya kaki upana nch 18 mifuko mitatu mbele miwili na nyuma mmoja.(shamba dress)
- Socks nyeupe (pair 3)

WASICHANA

- ➢ Sketi mbili linda box mbele na nyuma, linda mbili kushoto na kulia: rangi ya light blue iwe ndefu na iachie nafasi ya sentimita 6 au nch 2.5 kutoka kwenye kiatu
- ➢ Mashati meupe mawili ya mikono mirefu
- ➢ Scarf rangi ya light blue
- ➢ Gauni mbili ndefu rangi ya dark blue (kitambaa kizito) zenye kola nyeupe na mshono wa solo.(shamba dress)
- ➢ Sweta mbili (2) rangi ya kijani jeshi.
- ➢ Track suit 2 za kijivu.(isiwe na kofia)kwani hali ya hewa ya mtwango ni baridi kali
- ➢ Hijabu rangi nyeupe isiyo na urembo
- ➢ Socks nyeupe (pair 3)

- Soksi jozi mbili za rangi nyeusi za michezo
- Raba/viatu, bukta na jezi ya blue (muhumu sana)
- Koti jeupe lenye mikono mirefu (Laboratory coat) kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi tu.

**NB:** Mwanafunzi anapokuja shule aje akiwa amevaa track suit ya kijivu iliyoandikwa hapo juu.

**SURUALI ZA MITUMBA NA JEANS HAZIRUHUSIWI HAPA SHULENI.**

**MASHARTI MENGINE**

- i. Mwanafunzi asije shuleni na nguo nyingine zaidi ya zile zilizoagizwa vinginevyo atarudishwa nyumbani.
- ii. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa mlinzi wa mwenzake kuzuia uovu unaoweza kutokea katika chumba chao. Uharibifu wowote ule ukitokea/ukibainika katika chumba kimoja wapo wanafunzi wanaoishi katika chumba hicho wataadhibiwa wote, kwani wote watakuwa wameshiriki katika uharibifu wa mali ya umma. Mfano kuunganisha umeme kuchoma bweni, kuiba vitu nk.
- iii. Uharibifu wowote utakaosababishwa na wanafunzi ni jukumu la mwanafunzi na mzazi/mlezi kugharamia matengenezo.

NB: Endapo mwanafunzi atafanya uharibifu wowote wa mali za shule mfano; kuchoma moto majengo ya shule, kuharibifu madawati, kuvunja vioo, kuchora kuta za shule; mzazi/mlezi utawajibika kulipa ikishindikana mtoto wako atafukuzwa shule na kushitakiwa.

## VIFAA VINGINE VINAVYOHITAJIKA SHULENI

- a) Madaftari makubwa kumi (10) aina ya “COUNTER BOOK” kuanzia 3 quire, kalamu za kutosha na mkebe.
- b) Toilet papers za kutosha (12 – 15) kwa mhula mmoja.
- c) Vitabu vya masomo aangalie orodha iliyoambatanishwa kwa kila somo. Anaweza kununua baadhi ya hivyo.

## MAWASILIANO TOKA KWA MZAZI /MLEZI

Maagizo yote yote ya fedha au mzigo vitumwe posta tu ambapo muhudumu wa shule anaweza kuchukua na kuleta shuleni. Mwanafunzi hataruhusiwa kwenda kuchukua. Aidha taarifa nyingine inayomhusu mwanafunzi mfano taarifa ya kufiwa itumwe kwa Mkuu wa shule na si kupitia kwa mwanafunzi. Taarifa kama hiii haitasikilizwa.

## USAFI BINAFSI:

Unatakiwa kuja shuleni na nywele fupi, usinyoe panki au upara, hairuhusiwi kufuga ndevu wala kucha. Aidha unatakiwa kuwa msafi na uoge mara kwa mara.

## UTUNZAJI WA MAZINGIRA NA USAFI

Unatakiwa utunze mazingira ya shule katika hali ya ubora nausafi.

## USHIRIKI KAZI ZA MIKONO

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kazi za mikono ambazo zina lengo la kuendeleza elimu ya kujitegemea pamoja na kuimarisha afya ya mwili.

## NIDHAMU

Ili uweze kujifunza na kufaulu katika masomo yako unatakiwa kuwa na nidhamu ya hali ya juu. Unatakiwa kuzisoma na kuzielewa vizuri sharia za shule zilizoambatanishwa nyuma ya fomu hii. Pia ifahamike kuwa si jukumu la shule kutoa nauli pindi mwanafunzi anapopatikana na makosa ya kinidhamu ya kumrudisha nyumbani. Ni wajibu wako mzazi au mlezi.

## MICHEZO NA UTAMADUNI

Unatakiwa kushiriki michezo na utamaduni kwa lengo la kuleta uhusiano mwema na kujenga miili yenye afya. Jitokeze na ibua kipaji chako katika fani mbali mbali mfano: mpira, kuimba, kuigiza, skauti na kadhalika.

## DINI

Kila mwanafunzi anaruhusiwa kufanya ibada kulingana na imani yake ili mradi shughuli hizo zinaendeshwa kufuata sheria za nchi na ratiba ya shule. Aidha mwanafunzi atasali/swali shuleni na maeneo yaliyo karibu nashule.

## CHAKULA MAALUMU

Shule haitatoa chakula maalumu kwa wanafunzi tofauti na wengine. Aidha mzazi/mlezi unashauriwa umtafutie mahali ambapo ataweza kusoma na kupata huduma ya chakula kulingana na tatizo lake. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Nakutakiwa maandalizi mema na safari njema ya kuja MTWANGO SEKONDARI.

**KARIBU SANA**

**MKUU WA SHULE**

Nakala kwa:-

1. Katibu Mkuu,
   Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
   S.L.P 1923,
   **DODOMA.**

2. Katibu Tawala za mkoa
   S.L.P 668,
   **NJOMBE.**

3. Mkurugenzi Mtendaji,
   S.L.P 547,
   **NJOMBE.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI

**A: MWANAFUNZI**

1. JINA KAMILI…………………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………………………………….
3. Mahali alipozaliwa ………………………………………………………………………..
4. (Wilaya)………………………… (Mkoa) …………………………………………………..
5. Dini ……………………………………………………………………………………..
6. Dhehebu ……………………………………………………………………………..

**B: MZAZI/MLEZI ANAYEKUTUNZA**

JINA……………………………………………………………………………………………
KAZI …………………………………………………………………………………………..
ANUANI ……………………………………………………………………………………
ANAPOISHI
Wilaya …………………… Kijiji …………………………………… Kata …………………………………..

**C: JINA LA ANAYEKULIPIA ADA/KARO YA SHULE**
JINA…………………………………………………………………………………………… UHUSIANO ……………………………………..
ANUANI ……………………………………………………………………………………
SIMU …………………………………………………………………………………………..

**D: AFISA MTENDAJI/KATIBU KATA**
JINA……………………………………………………………………………………………………
KATA…………………………………………..Wilaya ………………………….Mkoa……………………
Nathibitisha kuwa mwanafunzi ………………………………………………………ni mkazi wa kata hii na ni raia wa Tanzania.
SIMU …………………………………………………………………………………

Sahihi ……………………………………………Muhuri ……………………….tarehe …………………

**JINA LAMWENYEKITI WA MTAA/KIJIJI**
JINA……………………………………………………………………………………………………
MTAA/KIJIJI ……………………………………………..KATA ………………………….WILAYA…………………… MKOA ……………….
Nathibitisha kuwa mwanafunzi ………………………………………………………ni mkazi wa mtaa/kijiji hiki na ni raia wa Tanzania.
SIMU …………………………………………………………………………………

# FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

## I. MWANAFUNZI

1. Mimi…………………………………………………........... kidato cha …………………......................
2. Nakubali kujiunga na shule hii ya Sekondari MTWANGO nikiwa mwanafunzi wa Bweni/Hosteli.
3. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote, sharia na taratibu zote za shule.
   Nimekubali kuingia kidato cha tano katika shule ya Sekondari MTWANGO.
4. Kwahiyo naahidi kwamba:-
   a) Nitazitii sharia zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu.
   b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vile ambavyo vita kuwa kinyume na uongozi wa chama tawala na Serikali ya Jamuhuri ya Muunganoawa Tanzania.
   c) Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na mazingira, samani (furniture), vitabu n.k
   d) Nitasoma kwa bidii na juhudi ili nifaulu.
   e) Nitashiriki katika shughuli zingine za nje mbali na masomo ya darasani.

Sahihi ya mwanafunzi………………………………………………… tarehe ………………………………………………

## II. JINA LA MZAZI/MLEZI

Mimi ……………………………………………………………………………….. ninakubali mtoto wangu ………………………………………………………………… kidato cha ……………………………… mwaka 2022 tarehe ………………………………… akiwa mwanafunzi wa Bweni/Hostel.

Kwahiyo naahidi:-

a) Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule walimu na wafanyakazi wengine katika kumuelimisha na kumkemea mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sharia na taratibu zote za shule na kuyatimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hao juu.
b) Nitafanya kila niwezalo ili kumwezesha mwanangu kufika shuleni mapema, kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufaulu kwa muda wote awapo shuleni.

Anuani yangu ya kudumu ni ……………………………………………………………………………………………………………

Sahihi ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………………………………… tarehe ………………………………

## III. KUWATEMBELEA WANAFUNZI/SIKU YA WAGENI

Wazazi / walezi wataruhusiwa kuwatembelea wanafunzi mara moja kwa mwezi ambao ni kila Jumapili ya kwanza ya mwezi kuanzia saa 8:00 mchana hadi saa 10:30 jioni. Mwalimu wa zamu atakuwepo shuleni kwa muda huo kupokea wageni; hairusiwi kumletea mwanafunzi chakula.

## ORODHA YA VITABU

**A. KISWAHILI**

1. nadharia ya lugha masebo, j.
2. kiswahili kidato cha 5 &6 oxford university press
3. nadharia ya fasihi masebo, j.
4. tahakiki

**B. ENGLISH LANGUAGE**

1. advanced english language oxford
2. english language nicholaus ashel
3. literature in english

**C. GEOGRAPHY**

1. physical geography msabila
2. human economic geography msabila
3. physical geography monk house
4. physical geography bunnet
5. intergrated geography david wash

**D. HISTORY**

1. advanced learner's history 5 & 6 oxford
2. masterial history carter
3. history for advanced zisti kamile

**E: CHEMISTRY**

1. Advanced Chemistry Review by William W. Davis (Mzumbe bookshop project, 2004)
2. Physical chemistry by Delungu, et (Mzumbe bookshop project, 1998)
3. Advanced Level Inorganic Chemistry part I and II. (Tanzania institute of education, 1995)
4. Organic Chemistry volume I. The Fundamental Principles by I.L Finar (Longman Ltd 1990)

**F: BIOLOGY**

Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia

1. New understanding Biology b Suzan Toole
2. Advanced Biology by Michael Kent
3. Biological science third by D.J. Taylor, N.P.O Green and G.W.stout.
4. Advanced Biology Principle and application by C.J Clegg and DG Mc Kean.
5. New understanding Biology for advanced level by Glenn and Susan Toole.
6. Plant and Animal Biology volume 1 & 2 by AE vines and N Rees.
7. Biology for class XI & XII by Dr. P.S Verma and Dr. B.P Pandey.

**G. GENERAL STUDIES**

1. General studies for A – level certificate form V.
2. Contemporary approach for A level general studies notes for form V and VI.
3. General Studies Supplementary Book for A level and Colleges.
4. Advanced level general studies notes form V & VI by Nyambari Nyangwine 2009

## SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana na Elimu nchini. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara tu anapowasili shuleni:-

a) Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi,wanafunzi wenzie na jamii kwa ujumla
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli( shughuli za kitaaluma na kazi za nje)

c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni(evening preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
h) Lugha chafu,matusi,ugomvi,fitina,kupiga/kupigana ni mwiko kabisa kwa mwanafunzi.
i) Wizi wa aina yeyote ni mwiko kwa mwanafunzi.
j) Unywaji wa vileo,kuuza pombe na uvutaji wa aina yeyote ni mwiko kwa mwanafunzi
k) Kuvaa sare za shule wakati wote unapokuwa shuleni((nguo zingine nje ya sare/maagizo ya shule haziruhusiwi)
l) Uharibifu na upotevu wa mali binafsi na mali za umma ni kosa na utawajibika kulipa mali husika
m) Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa akiwa bado mwanafunzi. Akibainika atafukuzwa shule mara moja. Aidha ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na uhusiano wa kimapenzi. Akibainika atafukuzwa shule.
n) Wageni wataruhusiwa kuwaona /kuonana na wanafunzi baada ya kujitambulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu kila jumapili ya mwisho wa mwezi tu.
o) Ni mwiko kwa mwanafunzi yeyote kwenda nyumba za walimu na wafanyakazi bila ruhusa ya pekee kutoka kwa mwalimu mlezi.
p) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na au kifaa chochote kinachohusiana na simu ya mkononi.
q) Mgomo wa aina yeyote ni marufuku na ni haramu.
r) Mwanafunzi atapokea maelekezo yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
s) Mwanafunzi atajisafirisha mwenyewe wakati wa likizo au pale atakaporudishwa nyumbani/kufukuzwa shule.

## MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE.

i. Wizi.

ii. Uasherati,ushoga,ubakaji,kuoa au kuolewa

iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama cocaine,kubeli nk.

iv. Uvutaji wa sigara.

v. Kupiga au kupigana kwa mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote na makosa mengine ya jinai.

vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

vii. Kudharau bendera ya Taifa.

viii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako,walimu au walezi na jamii kwa ujumla

ix. Kugoma kuchochea au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

x. Kukataa kwa makusudi adhabu.

xi. Kumiliki simu ya mkononi shuleni.

xii. Kushiriki au kuendeleza imani za kishirikiana

xiii. Kunyanyapaa au uonevu wa aina yeyote

xiv. Kuweka mimba au kupata mimba

xv. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 60 bila taarifa/utoro

xvi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

xvii. Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kama kunywa sumu n.k.

# FOMU NA.3. MEDICAL EXAMINATIONS.

(To be completed by medical officer only)

1. Pupil's name ……………………………………………………………………………………………….
2. Age…………………………………………………………………………………………………………..
3. Blood count (white and red)……………………………………………………………………….
4. Stool examination ……………………………………………………………………………………..
5. Syphilis or/and other venereal diseases test …………………………………………………
6. T.B test ……………………………………………………………………………………………………..
7. Eye test …………………………………………………………………………………………………….
8. Ears ………………………………………………………………………………………………………….
9. Abdomen …………………………………………………………………………………………………
10. Spleen ……………………………………………………………………………………………………..
11. Urine for plamo test ………………………………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION

If any e.g physical defeats, impairment, infections, pregnancy, chronic or family diseases etc ………………………………………………………………………………………………………………………………………………

I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION

STATION……………………………………………………………………………………SIGNATURE………………………….

DATE…………………..DESIGNATION……………………………………OFFICIAL STAMP……………………………..